

Toleo la. 16


Jarida la *Ni Magufuli Tena*

2020 - 2025

ALIAHIDI | AMETEKLEZA | APEWE TENA 5 | 17 SEPTEMBER, 2020



MAGUFULI ATINGA KIGOMA KWA KISHINDO



Limeandaliwa na **TEAM MAGUFULI TENA**

TAHARIRI

HOJA YA MAENDELEO YA WATU NA VITU NI MUFLISI

Baadhi ya viongozi wa vyama pinzani wamekuwa wakiwahadaa wananchi kwamba Serikali ya Chama cha Mapinduzi chini ya Dkt John Pombe Magufuli, imeleta maendeleo ya vitu na si ya watu.

Mjadala huu tunasema ni muflisi kwa sababu hauna mantiki yoyote katika uhalisia. Hakuna maendeleo yanayohusu watu bila kuweka miundombinu muhimu ambayo ni vitu.

Hii ya vitu na watu ni nahau tamu isiyo na maana yoyote na hata matukio ya viongozi wenyewe wa upinzani kuonekana kupita kwenye barabara zile zile, madaraja yale yale wanayoyaponda na hata kupanda ndege zile zile wanazoponda au kutumia viwanja vya ndege wanavyovipinga, wanapopita kwenda Ulaya, ni ushahidi kuwa nahau hii sasa imezikwa rasmi.

Imezikwa rasmi kwa sababu hata wapinzani wenyewe sasa wanaonekana kuiasi na kila siku wanatumia "vitu" hivyo hivyo kujipatia "maendeleo" yao kwa kuwezesha kufanya shughuli zao za siasa.

Tumemuona Tundu Lissu amerejea nchini na kupita kwenye Uwanja wa Kimataifa wa Julius Nyerere, Terminal III, Dar es Salaam. Akashangaa shangaa na kufurahia uwanja ule.

Juzi tu mgombea wa ACT ametokomea ughaibuni akipita kwenye uwanja huohuo ambao ni "kitu" kilichomsaidia kwenda nje.

Zitto Kabwe amesema sana kuwa ndege si maendeleo, sasa ghafla juzi hakupanda mawese kwenda kwao Kigoma bali kapanda Bombardier.

Ndio maana sisi tunaendelea kuisitiza kuwa Serikali yetu isisite kuendelea kuwekeza na kujenga miundombinu kwani kwa sasa mjadala wa dhana potofu ya watu na vitu umefungwa rasmi.





BARABARA YA NYAKANAZI HADI KIGOMA SASA KUWEKWA LAMI

Na Mwandishi Maalum - KIGOMA

Mgombea Urais kupitia Chama cha Mapinduzi (CCM) na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. John Pombe Magufuli ameendelea na kampeni za Urais akiwa njiani kuelekea Kigoma, amesimama wilaya ya Kibondo mkoani Kigoma na kuwaeleza wananchi kuwa shilingi bilioni 300 zitatumika kujenga barabara Nyakanazi, Kibondo, Kasulu hadi Kigoma yenye urefu wa kilomita 310 kwa kiwango cha lami.

“Naomba mnichague kwa kipindi cha pili cha miaka mitano, mchague na Mbunge wa CCM na madiwani wa chama chetu ili tukamilishe ujenzi wa barabara hii ambao tayari umeanza, wakandarasi wamepatikana, jukumu lenu kutupa muda wa kukamilisha kazi tuliyoanza” alisisitiza.

Rais Dkt. Magufuli amesema kukamilika kwa barabara hiyo kutiunganisha Kigoma

na mikoa mingine sambamba na mataifa jirani hivyo kuchochea maendeleo zaidi ya mkoa huo kwa kurahisisha usafiri wa watu na bidhaa.

Kuhusu miradi ya maji amesema kuwa zaidi ya shilingi bilioni tatu zinatumika kukamilisha mradi utakaotatua changamoto ya maji katika vijiji vya wilaya ya Kibondo na kwamba milioni 600 zinatumiwa kutekeleza mradi wa kutatua changamoto ya maji Kibondo mjini hivyo kuleta maendeleo ya watu wilayani humo. Sambamba na hayo, Rais Dkt. Magufuli amesema Serikali imejenga vituo vitatu vya afya, imepanua zahanati tatu pamoja na kukarabati shule mbili wilayani humo. Ameongeza kuwa vijiji 43 vimefikwa na umeme katika wilaya ya Kibondo ambapo aliomba apigiwe kura za kutosha ili amalie vijiji saba vilivyobaki ndani ya muda mfupi baada ya kuchaguliwa tu.



CHANGAMOTO YA MAJI KAKONKO SASA HISTORIA

Na Mwandishi Wetu - **KAKONKO**

Changamoto ya upatikanaji wa maji katika wilaya ya Kakonko mkoani Kigoma imepatiwa ufumbuzi baada ya kukamilika kwa mradi wenye thamani ya shilingi bilioni 4.69.

Hayo yamesemwa leo na mgombea Urais kupitia Chama Cha Mapinduzi (CCM) na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. John Pombe Magufuli alipozungumza na wakazi wa wilaya hiyo alipokuwa njiani kuelekea Kigoma mjini.

“Tumetekeleza miradi mingi ya maendeleo hapa Kakonko ikiwemo kuchimba visima katika vijiji 11 vya Wilaya hii, pia tumejenga hospitali ya Wilaya itakayokuwa na uwezo wa kufanya upasuaji” Alisema .

Kuhusu huduma za afya, Dkt. Magufuli amesema kukamilika kwa hospitali ya wilaya hiyo kutatatua changamoto kubwa ya wananchi kusafiri umbali mrefu kufuata huduma za upasuaji na kwamba vituo vya afya vimejengwa na vingine vimefanyiwa maboresho lengo likiwa kuimarisha huduma za afya kwa wakazi wa Kakonko.

Alipozungumzia miundombinu ya usafirishaji, alisema kujengwa kwa barabara ya Nyakanazi, Kibondo na Kasulu kutachangia kwa kiwango kikubwa katika kuchochea maendeleo ya Wilaya hiyo na Kigoma kwa ujumla.



MAENDELEO YA VITU YAIPAISHA CCM ITILIMA

Na Mwandishi Maalum - **SIMIYU**

Wakazi wa wilaya ya Itilima mkoani Simiyu, wamekihakikishia ushindi wa kishindo Chama Cha Mapinduzi (CCM) katika uchaguzi mkuu unaotarajiwa kufanyika Oktoba 28, 2020 kwa sababu ya maendeleo makubwa ya vitu ambayo wanasema yamesaidia kuinua maisha yao.

Hayo yameelezwa na wakazi wa Kijiji cha Igangabilili wilayani humo ambapo wamesema kwamba Rais Dkt John Magufuli ametekeleza miradi mingi ambayo haikwepo kabla hajashika madaraka.

Mmoja wa wakazi hao, Bw. aganda Shija amesema: "Mpaka sasa tunapata pembejeo za kilimo bure, na masoko ya uhakika ya pamba yameboreshwa, sioni sababu ya

kutoichagua CCM, najivunia kuona Mgombea Urais kupitia CCM ni Dkt. Magufuli".

Aidha, Kwa upande wake Bi. Winifrida Charles amesema licha ya kutokea familia duni amefanikiwa kumaliza kidato cha nne bure kutokana na mfumo wa elimu bila malipo ulioanzishwa na Serikali ya Awamu ya Tano.

Akihutubia mamia ya wakazi wa wilaya ya Itilima Mjumbe wa Kamati Kuu CCM Majaliwa Kassim Majaliwa amesema mpaka sasa Serikali ya CCM chini ya Dkt. John Pombe Magufuli imeshatoa shilingi bilioni 9.3 ili kukamilisha huduma ya maji kwenye makao makuu ya wilaya ya Itilima.



MWINYI KUTATUA CHANGAMOTO ZA WAFANYABIASHARA ZANZIBAR

Na Mwandishi Maalum - **PEMBA**

Mgombea Urais wa Zanzibar kupitia Chama Cha Mapinduzi (CCM) Dkt. Hussein Ali Mwinyi amewahakikishia wafabiashara wa kisiwa cha Pemba kwamba endapo atachaguliwa kuwa Rais wa Zanzibar atazishughulikia changamoto mbalimbali zinaowakabili wafanyabiashara.

Dkt. Mwinyi amebainisha hayo leo alipozungumza na wafanyabiashara katika ziara yake yakuwatembelea wafanyabiashara wa maduka mbalimbali kwenye mitaa ya mji wa Chake-Chake, Mkoa wa Kusini Pemba.

Wakati huohuo, Dkt. Mwinyi amezungumza na wavuvi, wafugaji wa samaki na wakilima wa Mwani ambapo amewahakikishia kwamba Zanzibar ataunda Wizara ya Uvuvi inayojitegemea tofauti na ilivyo hivi sasa kwasababu uvuvi ni shughuli kubwa ya kiuchumi inayomgusa kila Mzanzibari.

Sambamba na hayo, amesema endapo atashika hatamu ya kuiongoza Zanzibar atahakikisha anaweka mazingira mazuri ya uwekezaji wa zao la mwani kwa lengo la kuinua uchumi wa wakulima wa zao hilo na kwamba atahakikisha wawekezaji kutoka nje ya nchi wanajenga kiwanda cha zao hilo kisiwani Pemba.

Pamoja na hayo, Dkt. Mwinyi amewahakikishia wafugaji samaki kwamba atawaleta wataalamu wa ufugaji wa sekta hiyo kutoa mafunzo ili wafuge kwa tija huku akisema kwamba atatafuta masoko ya kutosha ili wanaofanya shughuli hiyo wanufaike na kazi yao.

5 KALI ZA MAGUFULI AKIWA NJIANI KUELEKEA MKOANI KIGOMA SEPTEMBER 17, 2020

01

Tunatekeleza mradi wa maji wenye thamani ya shilingi bilioni 4.69 hapa Kakonko na pia mradi wa kuchimba visima virefu katika Vijiji 11 unatekelezwa. Kukamilika kwa miradi hii kutafanya changamoto ya maji kuwa historia.

02

Tumetekeleza miradi ya maji yenye thamani ya shilingi bilioni 3 maeneo ya vijijini katika wilaya ya Kibondo, Pia kuna mradi wa kuboresha miundombinu ya maji kwa ajili ya Kibondo mjini kwa gharama ya shilingi milioni 600.

03

Jumla ya shilingi bilioni 300 zitatumika kukamilisha kwa kiwango cha lami ujenzi wa barabara ya Nyakanazi - Kibondo - Kasulu yenye 310 na ile ya Kasulu Manyovu. Tucha-
gueni tukakamilishe kazi hii.

04

Wilaya hii ya Kakonko ni mpya hivyo mkituchagua tutaipa kipaumbele cha pekee, tupeni kura ili tuje tuifanye makubwa katika wilaya hii.

05

Tunahitaji kuijenga hii nchi, ninyi hapa Kibondo ni masha-
hidi wa jinsi nchi zinazotuzunguka wananchi wake walivyopata shida kwa mauaji yaliyotokea, ni kwa sababu ya ubishi. Sasa nawaomba watu wa Kibondo na Watanza-
nia kwa ujumla ugonjwa wa majirani zetu usiwaingie kwani madhara yake ni makubwa.



MAGUFULI AANIKA MAFANIKIO MULEBA

• **Bilioni 65 Zimeteketeza Miradi ya Maendeleo**

Na Mwandishi Maalum - **KAGERA**

Katika kipindi cha miaka mitano iliyopita Serikali ya Awamu ya Tano imeteketeza miradi ya maendeleo yenye thamani ya shilingi bilioni 65.32 katika wilaya ya Muleba mkoa wa Kagera kwenye sekta za elimu, maji, umeme, barabara, uvuvi, na mpango wa kupunguza umasikini.

Mgombea wa Kiti cha Urais kupitia Chama Cha Mapinduzi (CCM), Dkt. John Pombe Magufuli ameyataja mafanikio hayo leo alipokua akiomba kura kwa wakazi wa wilaya Muleba na kuelezea kuwa katika sekta ya elimu, shilingi bilioni 9.946 zilitolewa kugharamia elimu bila malipo na jumla ya shilingi bilioni 8.4 kufanya ujenzi, ukarabati na ukamilishaji wa miundombinu ya elimu.

“Kuhusu maji tumeteketeza miradi yenye thamani ya shilingi bilioni 4.2 kwenye maeneo mbalimbali ya wilaya hii. Aidha, tumefikisha umeme katika vijiji 124 kwa shilingi bilioni 5.4, vimebaki vijiji 42 tu. Katika miradi ya miundombinu, barabara zenye urefu wa kilomita 18 zimejengwa kwa kiwango cha lami ikiwemo ya Muleba-Kanyambogo, Muhutwe-Luhanga, barabara za mjini zenye urefu wa kilomita 3.7 pamoja na bandari ya Katembe.

Akizungumzia sekta ya uvuvi na masoko, Rais Dkt. Magufuli amesema: “Tumetengeneza jengo la kupokea na kuhifadhi mazao ya samaki, pia tumejenga soko la kisasa la ndizi hapa Muleba Mjini pamoja na skimu za umwagiliaji.

Akieleza kuhusu jitihada za kupunguza umaskini Muleba, amesema kupitia Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF), Rais amesema jumla ya shilingi bilioni 12.6 zimetolewa, na mpango huo utaendelea, hivyo amewaomba watu wa Muleba wamchague kwa kura nyingi ili kupitia CCM afanye mengi zaidi katika miaka mitano ijayo.

“Najua kuna changamoto katika zao la Kahawa na tumeshaanza kulifanyia kazi, tunataka tuyamalize matatizo ya kahawa moja kwa moja. Tumefanya mengi makubwa hatuwezi kushindwa changamoto za zao hilo hivyo, naomba mtuamini, tumejipanga kufanya makubwa zaidi”, amesisitiza Rais Dkt. Magufuli

Kuhusu ombi la kukamilisha kipande cha barabara chenye urefu wa kilomita 5.8, Rais Magufuli amesemaalitoa ahadi hii. “Sasa nawaahidi mkituchagua, mkandarasi aliyetengeneza hiyo sehemu nyingine ya barabara ataendelea na hizo kilomita zilibokia”.



MAGUFULI ANATOSHA URAIS DKT. BASHIRU

Na Mwandishi Wetu - **KAGERA**

Katibu Mkuu wa Chama cha Mpinduzi (CCM) Dkt. Bashiru Ali amesema wananchi wa mkoa wa Kagera hawana sababu ya kuacha kumchagua mgombea Urais kwa tiketi ya Chama hicho na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. John Pombe Magufuli kutokana na kazi nzuri anayofanya ya kuleta maendeleo.

Dkt. Bashiru ametoa kauli hiyo leo kwenye mkutano wa kumuomba kura Dkt. Magufuli katika Jimbo la Bukoba Vijijini ambapo amewaomba wananchi wa mkoa huo wakiwemo wajasiriamali, wafanyakazi, wakulima na wafugaji kumpa kura za kishindo mgombea huyo, wabunge na madiwani wa CCM.

"Rais Magufuli ni kiongozi asiyebadilika kwa utendaji mzuri, amejenga Meli ya MV Victoria na kukarabati Meli tano, hivi sasa usafiri kati ya hapa Bukoba na Mwanza ni rahisi na hata usafirishaji wa mizigo umekuwa rahisi," amesisitiza Dkt. Bashiru.

Amefafanua kwamba Rais Magufuli amejenga miundombinu ya kisasa ya barabara, madaraja, Shule, viwanja vya ndege, hospitali, madaraja, vituo vya afya na zahanati na miundombinu mingine sambamba na ununuzi wa ndege.

Dkt. John Pombe Magufuli anaendelea na kampeni za kuomba kura kwa wananchi wa mkoa wa Kagera baada ya kukamilisha kampeni zake katika mkoa wa Geita na Kanda ya Ziwa.



MASOKO YA KIMKAKATI KUWAPAISHA KIUCHUMI WAJASIRIAMALI

Na Mwandishi wetu - SINGIDA

Mgombea Urais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia Chama cha Mapinduzi (CCM) Rais Dkt. John Pombe Magufuli ataendeleza ujenzi wa masoko ya kimkakati katika maeneo ya mipakani ili kuwapa wakulima, wajasiriamali wadogo hususan wanawake na vijana fursa ya kuuza mazao yao nje ya nchi.

Hayo yamebainishwa katika Ilani ya Chama cha Mapinduzi (CCM) hicho ya mwaka 2020-2025 ambayo pamoja na mambo mengine, itawaunganisha wazalishaji, wasindikaji na wafanyabiashara kwenye masoko ya ndani na nje ya nchi kupitia mifumo maalum.

“Serikali itaandaa na kutekeleza mikakati ya upatikanaji wa mitaji kwa ajili ya kuimarisha na kukuza biashara ndani na nje ya nchi na pia kubuni na kuendeleza mikakati ya uhamasishaji ili watanzania wapende kutumia bidhaa zinazozalishwa katika viwanda vya ndani,” Inaeleza Ilani hiyo.

Aidha, Rais Dkt. Magufuli ataweka mazingira wezeshi ya biashara na kuhakikisha kwamba fursa za biashara zinapatikana ili kuchochea ujenzi wa viwanda na uzalishaji wa bidhaa zenye ubora wa kimataifa na zinazostahimili ushindani.

Sambamba na hayo, mgombea huyo ataitekeleza Ilani ya CCM ambayo inaahidi kuimarisha majadiliano ya biashara ya kikanda na kimataifa ili kuongeza fursa mbalimbali za ufanyaji biashara kwa bidhaa zinazozalishwa nchini ikiwa ni pamoja na kuhamasisha sekta binafsi kuchangamkia fursa.

Katika muhula wake wa kwanza, Rais Dkt. Magufuli ameiwezesha Tanzania kuingiza zaidi ya dola za Kimarekani milioni 288 kwa kuuza mazao mbalimbali katika mataifa ya Afrika Mashariki.



UKARABATI WA UWANJA WA NDEGE RUVUMA WAKAMILIKA

• Ndege Kuanza Kutua Mwezi Oktoba

Na Mwandishi wetu - RUVUMA

Mgombea Mwenza wa Urais kupitia Chama Cha Mapinduzi (CCM) ambaye pia ni Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Samia Suluhu Hassan amesema uwanja wa Ndege mkoani Ruvuma uliokuwa ukijengwa na kukarabatiwa kwenye baadhi ya maeneo umekamilika na ndege zitaanza kutua mwanzoni mwa mwezi mwa Oktoba, mwaka huu.

Samia amesema kukamilika kwa ujenzi huo ni juhudi za Serikali ya Awamu ya Tano ya Rais Dkt. John Pombe Magufuli za kuimarisha miundombinu ya usafirishaji mkoani Ruvuma na Tanzania kwa ujumla na hivyo kuwaomba wananchi wa mkoa huo wamchague tena Magufuli ili kwa kushirikiana nae katika nafasi yake ya Makamlu wa Rais, wkuhakikisha maendeleo zaidi yanapatikana.

"Ruvuma hapa tuliahidi na tumetekeleza, mchagueni Dkt. John Pombe Magufuli ili tushirikiane kuwaletea maendeleo mengi zaidi kwani yajayo yanafurahisha," amesema Mhe. Samia.

Katika hatua nyingine, Mhe Samia Suluhu Hassan amesema Serikali imetoa zaidi ya shilingi bilioni mbili kukarabati shule mbili kongwe za Songea Wasichana na ile ya Wavulana. Pamoja na ukarabati wa shule hizo pia Serikali ya Magufuli ilitoa zaidi ya shilingi bilioni 16 kukarabati shule za Msingi na Sekondari mkoani humo ili kuboresha elimu. Serikali ilitoa zaidi ya shilingi bilioni 37 kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa miundombinu.

ya Uwanja wa Ndege mkoa wa Ruvuma na sasa ujenzi wake umekamilika ambapo shilingi milioni 600 zinaandaliwa kwa ajili ya kulipafidia wakazi waliopisha ujenzi huo



SERIKALI KUIJENGA UPYA BARABARA YA MAKAMBAKO - SONGEA

• Bilioni 65 Zimetekeleza Miradi ya Maendeleo

Na Mwandishi Maalumu - **SONGEA**

Serikali ya Awamu ya Tano inayoongozwa na Rais Dkt. John Pombe Magufuli itaifumua na kuijenga upya kwa kiwango cha lami barabara ya Makambako hadi Songea yenye urefu wa kilomita 295, lengo likiwa ni kuepuka ajali, gharama na muda wa usafiri kwa watumiaji wa barabara hiyo.

Tayari Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS) wamekamilisha kazi ya upembuzi yakinifu, usanifu wa kina na utayarishaji wa nyaraka za zabuni hatua zitakazosaidia kufanikisha ujenzi wa barabara hiyo muhimu kwa uchumi wa Taifa.

Akizungumza wakati alipowahutubia wakazi wa Madaba Mkoani Ruvuma, Mgombea Mwenza wa Urais kupitia Chama Cha Mapinduzi (CCM) Mhe. Samia Suluhu Hassan amesema: "Ndugu zangu wa Madaba, Serikali yenu inayoongozwa na Rais Dkt. John Pombe Magufuli katika kipindi cha miaka mitano ijayo, inakusudia kuifumua na kuijenga upya barabara ya Makambako hadi Songea kwa kiwango cha lami ili kuleta maendeleo ya nchi pamoja na ya watu wa mikoa ya Kusini na nchi jirani, nawaomba sana mchaguenu tena afanikishe jambo hili," amesema Samia.

Mhe. Samia pia amesema Serikali inaendelea na mradi wa ujenzi wa barabara ya Mbinga-Mbambabai yenye urefu wa kilomita 67 kwa kiwango cha lami pamoja na kukamilisha ujenzi wa daraja la mto Ruhuhu, linalounganisha mkoa wa Ruvuma na Njombe.

Aidha, amezungumzia pia uboreshwaji wa miundombinu ya barabara zingine za mkoa huo ambazo zimekuwa ni kitovu cha kiuchumi, huku akitolea mfano barabara ya Ruvuma-Unyoni hadi Mbinga yenye urefu wa kilomita 25 na barabara ya Mpakani hadi Lingusenguse pamoja na nyinginezo ambazo zote zimewekwa kwenye mpango wa utekelezaji katika muhula ujao.

Katika Sekta ya Elimu, Mhe. Samia amesema kati ya shilingi bilioni 26.423 zilizotengwa kwa ajili ya kuhudumia miundombinu ya elimu na vifaa vya kujifunzia na kufundishia katika mkoa wa Ruvuma, Halmashauri ya Madaba iliyopo mkoani humo ilitumia shilingi bilioni 1.407 katika sekta hiyo na kwamba miundombinu muhimu imeboreshwa.

Aidha, ameahidi ujenzi wa vyuo viwili vikubwa vya ufundi stadi lengo likiwa ni kuwafundisha vijana wengi waweze kujiajiri.



MAJALIWA: WAPUUZENI WANASIASA WALAGHAI

Na mwandishi wetu - **SINGIDA**

Vijana wa Jimbo la Singida Kaskazini wametakiwa kuwapuuza wanasiasa walaghai na badala yake kuchagua viongozi bora kutoka Chama Cha Mapinduzi (CCM) ili washirikiane nao katika kuleta maendeleo.

Hayo yamejiri leo wakati Mjumbe wa Kamati Kuu ya CCM na Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Kasim Majaliwa akizungumza katika mkutano wa hadhara wa kuomba kura katika Wilaya ya Singida Vijijini.

"Wakiwaletea fedha kuleni lakini kura mpeni Rais Dkt. John Pombe Magufuli na Mbunge ni Ramadhan Ighondo wa CCM ndio atakuwa mwakilishi sahihi wa wanaSingida Kaskazini", alisema Mhe. Majaliwa.

"Wakiwaletea fedha kuleni lakini kura mpeni Rais Dkt. John Pombe Magufuli na Mbunge ni Ramadhan Ighondo wa CCM ndio atakuwa mwakilishi sahihi wa wanaSingida Kaskazini", alisema Mhe. Majaliwa.

Sambamba na hilo, baadhi ya vijana walioongea na mwandishi wa habari hii wamesema wameji-panga kumpa kura za kutosha Rais Dkt. Magufuli kwasababu amefanya kazi kubwa ya yakuwaletea maendeleo katika sekta zote.

Mbali na hayo, Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) Wilaya ya Singida Vijijini Frank Akunai amekiunga rasmi na CCM ikiwa ni hatua ya kuunga mkono juhudi zilizoletwa na Serikali ya Awamu ya Tano inayoongozwa na Rais Dkt. Magufuli.

Jarida la Ni Magufuli Tena

2020 - 2025



Limeandaliwa na **TEAM MAGUFULI TENA**